GLOBAL AFRICA

Wito wa Maombi

**PROGRAMU YA WATAFITI CHIPUKIZI, 11–17 DESEMBA 2022, NIAMEY, NIGER**

## MUKTADHA

Global Africa inatangaza wito wa maombi kwa programu ya kwanza ya **Taasisi ya Watafiti Chipukizi** (Junior Researchers' Institute, JRI), iliyoundwa kwa lengo la kuwashirikisha zaidi watafiti chipukizi na watafiti vijana katika uwanja mpana wa sayansi za jamii, hivyo kuwawezesha kushiriki na kuchangia kwa nguvu katika kuunda ujuzi mpya wa kimataifa.

JRI ni **sehemu ya msingi ya mradi wa Global Africa** unaopangwa na kusimamiwa kwa kushirikiana na washikiri wengine wa Global Africa, chini ya uangalizi wa *Laboratoire d'études et de recherches sur les dynamiques sociales et le développement local* (Maabara ya Mafunzo na Utafiti juu ya Mienendo ya Kijamii na Maendeleo ya Mitaa, LASDEL), maabara huru ya kikanda, yenye makao makuu mjini Niamey, Niger, pamoja na tawi katika mji wa Parakou, Benin.

## MADHUMUNI

*Taasisi ya Watafiti Chipukizi* (JRI) ilibuniwa kusitawisha uwezo wa watafiti chipukizi na vijana katika uandishi wa kisayansi na uchapishaji wa kitaaluma. Hususan, madhumuni yake ni yafuatayo:

- Kukuza uwepo barani Afrika wa watafiti wenye mafunzo madhubuti na uwezo wa kutoa makala mazuri zinazofaa kuchapishwa katika jarida la *Global Africa* au majarida mengine muhimu yenye kutambulika katika taaluma na kukidhi kiwango cha kitaifa na cha kimataifa.

- Kuunda kigezo cha mafunzo na maendeleo ya watafiti chipukizi kwa nia ya kuwaingiza na kuwawezesha kushiriki katika ulimwengu wa kitaaluma, wakiwa na elimu na uzoefu unaotakiwa katika muktadha za tafiti na taaluma zao. JRI inadhamiria kuchangia katika uimarishaji upya wa maarifa kuhusu Afrika, na kuwainulia hali wasomi chipukizi na watafiti, kwa kuchapisha kazi zao huku wakipatiwa mafunzo zaidi ya uandishi na ya uchapishaji wa kitaaluma, hayo yote yakifanyika katika mazingira ya kazi yenye kuwezesha maendeleo yao pamoja na mabadilishano ya kitaaluma.
- Kuunda mfumo thabiti kwa watafiti chipukizi kwa kuwapatia usaidizi endelevu, wakipatiwa ushauri maalum kutoka kwa wasomi wazoefu.

Kikao cha kwanza cha *Junior Researchers' Institute* kitafanyika Niamey, Niger na kuendelea kwa muda usiopunguwa wiki moja. Kikao kitahusishwa na toleo la tano la *Global Africa,* lenye kuzingatia mada ya **"Kuondoa Ukoloni katika Mustakbali ya Utendaji wa Umma Barani Afrika."**

Bila shaka, mada kama hii ambayo, kwa hakika, ni ya kusisimua, itawavutia na kuwahamasisha watafiti wanaodhamiria kuelewa mienendo ya dola inavyoumbwa na kuendelezwa barani Afrika. Leo, jinsi mada hii inavyohusisha mitazamo na taaluma za aina nyingi kwa wakati mmoja ni msingi maalum wa mijadala na chunguzi nyingi za sayansi za jamii. Kwa hivyo, kikao hiki kitawapa washiriki wanaochaguliwa nafasi ya kuchangia kwa kiwango cha juu katika mada ambayo, daima, ni ya msingi, na umuhimu wake kimkakati katika kuzungumzia na kutathmini dhana ya dola barani Afrika unatambulika.

## MAOMBI

JRI inawakaribisha watafiti wenye umri wa chini ya miaka 35, waliokwishamaliza shahada ya uzamivu katika sayansi za jamii au durusi za sanaa, au, watafiti wanaojiandaa kutetea tasnifu zao na wanaotarajia kuhitimu mwaka huu, na wana mpango wa kuandika makala inayoendana na mada ya toleo maalum la *Global Africa,* ambalo wito wake wa makala umeambantanishwa hapo chini.

Jalada la maombi lijumuishe:

- Barua ya maombi
- Wasifu wa mwombaji (C.V.)
- Mswada wa makala (maneno 3500–5000)

Kwa wanafunzi wa shahada ya uzamivu watakaotetea tasnifu zao mwaka huu (2022), uambatanishwe uthibitisho rasmi wa kwamba tasnifu imeshapokelewa, au, barua kutoka kwa mshauri mkuu wa tasnifu, yenye kutaja tarehe iliyopangwa kwa ajili ya utetezi.

**Maombi yapelekwe kwa Sekretariati ya Taasisi ya Watafiti Chipukizi kwa kutumia anwani ifuatayo ya barua pepe: school@globalafricasciences.org kabla ya tarehe 30 Oktoba 2022, saa 23:59 kwa majira ya GMT.**

Kuondosha ukoloni kwenye mustakabali
wa utawala wa umma barani Afrika

*GLOBAL AFRICA* – NUMBER 5, SEPTEMBA 2023

Kama ufuatiliaji wa toleo nambari 4, ambalo lilijikita kwenye kufafanuwa changamoto za ubinifu wa uelewa barani Afrika, toleo hili maalum la *Global Africa* linajielekeza kwenye fikira za kiepistemolojia, kinadharia na kimethodolojia na makisio juu ya somo la **Utawala wa Umma Afrika**. Jarida hili kuutilia mkazo maalum uchambuzi wa masuala ya kilimwengu kwa mtazamo na maslahi ya Afrika kwenye mada ya utawala wa umma hakuepukiki. Mbali ya maslahi mapya ya tafiti kwenye miaka ya hivi karibuni katika somo ambalo awali lilikuwa likidharauliwa kwa muda mrefu (kwa mfano, kama inavyoonesha katika tafiti zilizoongozwa na taasisi ya Transnational Research Group (TRG) juu ya "Umangimezeshaji wa jamii za Kiafrika" (2017-2021)1.), hatuna budi kuchambuwa kwa undani utawala wa umma barani Afrika. Hapa tuna mteremko muhimu na usioepukika (kwani unakwenda mbali zaidi ya usimamizi kwa maslahi ya pamoja) kwa ajili ya kuwachunguza na kuwafahamu watendaji wa utawala serikalini wanaonaswa baina kufuata mfumo wa uliberali mamboleo, kuzishughulikia changamoto za zamani, na kukabiliana na masuala yanayoibuka kila siku ya matakwa mapya yanayovuuka mipaka ya mataifa. Changamoto ambazo zinaufanya mdahalo juu ya uwezo wa vyombo mbalimbali vya dola kutekeleza maamuzi ya masuluhisho uzuke upya, ama kupitia taasisi za mamlaka za dola (vyombo vya dola, polisi na mahakama) ama taasisi za utawala wa umma (kama vile hospitali, vyuo vikuu, …).

Hata kama utawala wa umma barani Afrika unakabiliana na changamoto hizi zisizotegemewa, bado kuna taasisi ambazo zimejengwa madhubuti kabisa juu ya mifumo iliyoingizwa kutoka nje (Badie 2002), uchache na upungufu (Anders 2010; Bako-Arifari

2001, 2006; Bayart, Hibou & Ellis 1997), ya utepetevu na nakisi (Cameron 2010; Bayart 1989), ugoigoi na kutokuwepo kwa utaratibu unaofaa (Darbon & Crouzel 2009). Kwa hakika, uchambuzi wa siku kwa siku wa utawala wa umma unaibuwa taasisi zilizovurugika kisiasa na kimangimeza na pia mazungumzo ya kuhodhi, na hata machafuko kwenye mahusiano baina ya utawala wa umma na watumiaji wake, na hivyo kuhakikisha kwamba changamoto za ufanisi, mgawanyiko, usawa na ujumuishaji ziko mbali sana kufikiwa. Hali hizi zinazoonekana kutozuilika zimehalalisha kuwepo kwa mfumo wa kudumu na wa shaghala-baghala wa mageuzi na msaada, ukiwa na matokeo halisi na ya ishara (Easterly 2010; Machikou 2013; Machikou Ngameni 2014; Darbon 1985, 1990).

Kwa kiwango gani mifumo ya kikoloni na kitamaduni kwenye utawala wa umma, na pia uendeshaji wa serikali ya kikoloni, inaleta athari kwa sasa? Ni namna gani watawala wa Kiafrika wanaweza kujiweka huru kutoka kwenye umangimeza wa kikoloni ili waweze kuvumbuwa njia nyingine? Alimradi, kujibu masuali haya, yaani, kutengeneza nadharia yakinifu kwa utawala wa sasa na ujao kunatakiwa pawepo – lakini sio pekee – haja ya kuamuwa athari kubwa na zenye pande nyingi za masalia ya (baada ya) ukoloni kwenye mataifa ya Kiafrika, ili, kwa msingi huu, kuchambuwa modeli mbadala za kuchukuwa nafasi yake na kuanzisha matendo mapya.

Toleo hili maalum linajikita kwenye kuweka sawa masuali haya yahusuyo uondoaji ukoloni na kuumba upya utawala wa Kiafrika katika siku zijazo. Baada ya yote, hili ni suala la kujaza zaidi ya ombwe, kwa sababu ikiwa tunatambua kwamba, kwa umuhimu wake, kwa kukimbilia kuondosha ukoloni wa mila za kitaasisi, wa epistemolojia, ontolojia, matendo, sera na michakato yake, lazima ufanyaji kawaida wa kuondosha mitazamo ya kikoloni nako kusionekane kama jambo la dhana tu.  Hakuna shaka kwamba mojawapo ya sehemu ambapo dhamira maalum ya kuondowa ukoloni, yenye machafuko na yenye uharibifu, iko mbali sana

kufikia ahadi zake ni hiyo ya taasisi za umma. Na bado, utawala wa umma unaonesha matatizo (makongwe na mapya) ambayo ndiyo miongoni mwa muhimu kabisa kutatuliwa, yakiwemo ya mamlaka na ufanisi wa kiutawala; maguezi makubwa kabisa ya sehemu ambazo zinazalisha ukosefu wa usawa, ubaguzi na ufisadi; ujenzi mpya wa mipaka ya kiutawala na umuhimu wa kijamii katika mipango ya kiutawala; uhusiano wa raia na Dola na taasisi za umma. Nyenzo gani za uchambuzi zinazoweza kutumiwa na zoezi hili ikiwa tunazingatia onyo la kiuchokozi la Audre Lorde dhidi ya masanduku ya zana za sayansi jamii ya kale: “silaha za bwana kamwe hazitaivunja nyumba ya bwana” (Lorde 1979, 1984)? Suala hili linawaalika wasomi kushiriki kwenye zoezi hili, ambalo linadhamiria kujenga upya mustakabali wa kuondosha ukoloni kwenye tawala za umma barani Afrika kwa kujikita kwenye michakato mitatu inayofungamana.

## 1. Kuwakwamuwa Watawala wa Kiafrika kutoka kwenye makucha ya maktaba ya kimangimeza

Kuondosha ukoloni kwenye tawala barani Afrika kunajumuisha, kwanza kabisa, uhakiki wa kina wa “maktaba ya kimangimeza” (TGR 2017-2021), yaani kile kiini cha uwelewa wa kisomi, uwakilishi, nyaraka, imani, utaalamu na mifumo ambayo umangimeza wa Kiafrika umejengewa. Tukichukuwa kutoka dhana ya Valentin Mudimbe ya “maktaba ya kikoloni”, utafiti wa “maktaba ya kimangimeza”, kama wasomi kutoka TRG wanavyokariri, “uchambuzi changamano”, kama ilivyo pia utaratibu wa epistemolojia, uzalishaji mwenza, mashirika ya kimataifa, ikiwemo Benki ya Dunia, lazima uzalishe, ugawanye, usambaze maarifa kuhusu utawala na maendeleo kwa kiwango kikubwa (Nay 2009:153).

Kuchukuwa mtazamo wa kuondosha ukoloni, kwa hivyo, pia kunamaanisha kuondosha ukoloni kwenye urasimu wa mashirika ya kimataifa, hasa yale yenye kuhusika na sera za mageuzi kwenye utawala na masuala ya maendeleo (Benki ya Dunia, Mfuko wa Fedha wa Kimataifa, IMF), Shirika la Biashara Duniani (WTO), yale ambayo yanatowa kanuni na mifumo, na vile vile malengo ya maendeleo kama vile Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs) na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), ambayo kwa kiwango kikubwa yanadhibitiwa na mataifa tajiri ya Jumuiya ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD). Kituko ni kwamba taasisi hizi zinapingana zaidi na mabadiliko na ukosoaji dhidi yao kuliko tawala ambazo zinafikiriwa kusaidiwa nazo (Nay 2009:160).

Vile vile, kuchukuwa mtazamo wa kuondosha ukoloni kwenye tawala za kiafrika (APAs) kunapelekea kwenye zoezi na upembuzi ambalo njia yake ya kuingilia inaweza kuwa suali lifuatalo: vipi tunaweza kufahamu muendelezo wa ukoloni na vipi tunalishughulikia suala la mfungamano baina ya mfumo wa ukoloni mamboleo/baada ya ukoloni na umangimeza wa kisasa (Bayart, Médard)? Dhamira hapa ni kubainisha mizizi ya (baada ya) ukoloni na ubovu ama ukosefu wa ubovu kwenye historia inayotandwa na udhibiti wa taasisi za kikoloni unaofanywa na tabaka jipya la watawala. Hili pia limaanisha kuhoji nyayo za moja kwa moja na za ishara za userikali wa (baada ya) ukoloni kupitia mifumo yake yenyewe. Kwa maneno mengine, inamaanisha kuuliza kwa ufasaha zaidi juu ya vipindi gani, kwenye sekta zipi na kupitia raia wapi ambapo mabaki ya ukoloni (mamboleo) yanaweza kuonekana. Kwa ajili na dhidi ya nani yanatekelezwa? Kwa mujibu wa mbinu ipi na athari gani? Kipi, kwenye mzozo wa kudumu wa APAs, ni matokeo ya mambo mengine?

## 2. Kuwakombowa watawala wa Kiafrika kutoka kushikiliwa mageuzi ya kudumu

Uchambuzi wa sekta ya utawala unaibuwa dunia iliyojaa watumishi wa umma, wafadhili, wataalamu, taasisi za jamii za nchi na nchi/mataifa, mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi za wasomi na washauri binafsi wenye vionjo vya uanamageuzi, itikadi, maadili na uelewa unaokinzana. Kwenye hali hii, mageuzi ya kudumu yamewekwa kama sharti la "misaada ya maendeleo" na kama mbinu ya usimamizi wa tawala za Afrika.

Kwa uundaji wa hili "soko la mageuzi", utegemezi wa kitaalamu unapigiwa chapuo, ukiunganishwa na mabadiliko ya kila siku kwenye mila, miongozo na kanuni za ufadhili ambazo zinahitaji mduara usio na ukomo wa ujenzi wa uwezo na mafunzo ambayo hayana mantiki wala hayatathminiwi. Matokeo haya ni "mkusanyiko ambao unazuwia aina yoyote ya umiliki na utaasisishaji, na moja kwa moja kuufanya utawala uwe wenye kuchanganya zaidi. Mageuzi ya kiutawala barani Afrika sio tu ni mengi, lakini pia yanagongana na kuzalisha misuguano au 'wanyama wakali' kwa kuunganisha, bila muakisiko, dhana na mbinu ambazo zote hazitangamani zaidi kwa sababu zinatekelezwa na mashirika tafauti ya nje na yanayoshindana", wanasisitiza Darbon na Crouzel (2009). Yote haya ni msingi wa mdahalo wa kwelikweli juu ya mamlaka ya watendaji wa kisiasa na kiutawala wa ndani, utwaaji wa miundo na mbinu zinazopendekezwa, na utekelezwaji wake kwenye mazingira yake ya kijamii.

Kwa hivyo ni suala la kuwakombowa watawala wajao wa Afrika kutoka kwenye maktaba ya urasimu na msukumo wa mageuzi kupitia chambuzi zilizojikita kwenye uwekaji wa tawala zinazoendana na mijengeko ya kijamii na kiuchumi zilizo makhsusi kwa nchi za Kiafrika, zenye kugusana na utambuzi wa kienyeji, mila za kitamaduni na taasisi za kijamii. Ujenzi wa kijamii wa rasimu uliojichimbia kwenye mazingira ya kijamii, kitamaduni na kiuchumi utawezesha kuunda utawala halisi wa Kiafrika na uzalishaji wa mfumo wa kikanuni ambao unazingatia kwenye mazungumzo na silaha kile Philippe Warin anachokiita "mmiminiko wa kijamii"

(2002), yaani, tahadhari ya sehemu kubwa ya umma, tafauti za kijiografia na kiuchumi, na pia huku kasi ya mageuzi ikiendelea kwenye demografia, muundo wa kuishi, kutumia, kufanya kazi na kuwasiliana. Hili ni suala la kufasili upya huduma zinazotaka kutolewa kwa umma, miundo ya utoaji wao, na maadili ambayo yanaelezea huduma za kijamii ili iwezekane kuanzisha tena mafungamano ya heshima, utu, usawa na ujumuishaji.

### 3. Kujenga utendaji mpya wa utawala wa Kiafrika

Mwisho, ili kuushinda mfadhaiko mkubwa (Stiglitz 2002), uondoshaji wa ukoloni unarejea pia kwenye utekelezaji wa kimantiki, ambazo masharti na matendo yake lazima yatambuliwe. Uvunjaji na ubomoaji wa kimfumo wa nyenzo za ukoloni (mamboleo) za usakaji, unyonyaji na ukatili, kama Yvette Mutumba anavyokariri, unahitaji "kubadilisha miundo kwa kiwango kile kile cha kujenga mipya" (Larios 2020). Mambo gani utawala ulioondoshwa kwenye ukoloni uwe nao na vipi yanaweza kufikiwa?

Michango ielekezwe kwenye kutambua baadhi ya miundo halisi kupitia utambuaji yakinifu wa masuala ya ufanisi, mgawanyo, usawa na ujumuishaji, na kupitia uvunjaji wa mifumo ya ghasia na ukandamizaji wa ndani na kimfumo kwenye miundo ya kisasa ya utawala.

Mjadala lazima ujikite kwenye miundo, misheni, na kazi ambazo utawala uliobuniwa upya lazima uzipeleke kwenye zama za kidijitali. Kwa mfano, kwa kiwango gani utawala wa kidijitali ni suluhisho kwa changamoto zote hizi?

## Selected Works

Anders, G., 2010, *In the Shadow of Good Governance. An Ethnography of Civil Service Reform in Africa,* Leiden, Brill.

Badie, B., 1992, *L'État importé. Essai sur l'occidentalisation de l'ordre politique*, Paris, Fayard.

Bako-Arifari, N., 2006, "'We don't eat the papers': corruption in transport, customs and the civil forces". In Blundo, Giorgio and Jean-Pierre Olivier de Sardan, Tidjani Alou M., eds. *Everyday Corruption and the State. Citizens and Public Officials in Africa,* London, Zed, 177–224.

Bako-Arifari, N., 2001, « La corruption au port de Cotonou : douaniers et intermédiaires », *Politique africaine,* n° 83, p. 38–58.

Bayart, J.-F., Ellis, S. et Hibou, B., 1997, *La criminalisation de l'État en Afrique*, Bruxelles, Complexe.

Bezes, P., 2008, « Construire des bureaucraties wébériennes à l'ère du New Public Management ? » *Critique internationale,* 35 (2) : 9–29.

Bierschenk, T., J.-P. Chauveau, J.-P. Olivier de Sardan (dirs), 2000, *Courtiers en développement. Les villages africains en quête de projets*, Paris, Karthala & APAD.

Cameron, R., 2010, « L'administration publique en Afrique. Introduction », *Revue internationale des sciences administratives*, vol. 76 : 637–643.

Cooper, F., 1996, *Decolonization and African Society: The Labor Question in French and British Africa,* Cambridge, Cambridge University Press.

Copans, J., « Afrique noire : un État sans fonctionnaires ? » *Autrepart*, n° 20, 2001 : 11-27.

Darbon, D., 1985, « Pour une socio-anthropologie administrative », *Revue française d'administration publique,* n° 35 : 457–468.

Darbon, D., 2015, « Des administrations africaines paradoxales : entre pratiques locales plurales et régimes d'aide incertains », *Quaderni,* n° 87 : 37–50.

Darbon, D., 1990, « L'État prédateur », *Politique africaine,* n° 39 : 37–45.

Darbon, D., 2014, « Bureaucratisation des réformes administratives et action publique en Afrique : l'enjeu de la repolitisation du projet administratif », dans *Espaces du service public ; mélanges offerts à Jean du Bois de Gaudusson*, Presses universitaires de Bordeaux.

Easterly, W., 2010, *The White Man's Burden: Why the West's Efforts to Aid the Rest Have Done so Much Ill and so Little Good,* Penguin Press, New York.

Fourchard, L., 2018, *Trier, exclure et policer. Vies urbaines en Afrique du Sud et au Nigeria*, Paris, Presses de Sciences Po.

Hagmann, T., Péclard, D., 2010, "Negotiating statehood. Dynamics of power and domination in Africa", *Development and Change* 41 (4): 539–562.

Larios, P., 2020, "Yvette Mutumba on Why Decolonizing Institutions 'Has to Hurt'", *Frieze*, June 06. URL: https://www.frieze.com/article/yvette-mutumba-why-decolonizing-institutions-has-hurt

Leguil-Bayart, J.-F., Bertrand, R., 2006, « De quel "legs colonial" parle-t-on ? », *Esprit*, n° 12 : 134–160.

Lorde, A., 1984, "The master's tools will never dismantle the master's house" (Comments given at the "personal and the political panel", at the Second Sex Conference, on September 29, 1979, in New York).

Luste Boulbina, S., « Décoloniser les institutions », *Mouvements,* n° 72, 2012 : 131–141.

Machikou, N., 2013, « L'entre-capture de la gratuité du service public judiciaire. Entre misère et distanciation », Hourquebie F. (Éd.), *Quel service public de la justice en Afrique francophone ?* Bruxelles, Bruylant : 165–174.

Machikou Ngameni, N., « La sédimentation d'une communauté de connaissance au cœur de l'action publique en Afrique. Un nouveau souffle pour les politiques publiques ? », dans Fabrice Hourquebie (Éd.), *La doctrine dans l'espace africain francophone*, Bruxelles, Bruylant, 2014 : 59–80.

Mudimbe, V., *L'Invention de l'Afrique. Gnose, philosophie et ordre de la connaissance*, Paris, Présence africaine, 2021.

Stiglitz, J., 2002, *La Grande Désillusion*, Paris, Fayard.

Williamsburg, V., 2006, "Dealing with the local state. The informal privatization of street-level bureaucracies in Senegal", *Development and Change* 37 (4): 799–819.

Williamsburg, V., 2001, « Négocier l'État au quotidien : intermédiaires, courtiers et rabatteurs dans les interstices de l'administration sénégalaise », *Autrepart* n° 20 : 75–90.